**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**
**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

# MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MACHI, 2019 NA MWELEKEO WA APRILI, 2019

**Dondoo za Machi, 2019**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Machi, 2019 na mwelekeo wa viashiria na matarajio ya mvua kwa mwezi Aprili, 2019 nchini.

a. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2019 maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalikumbwa na vipindi virefu vya ukavu husussan katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi, isipokuwa kwa maeneo machache ya kanda ya Ziwa Victoria ambayo vipindi vya mvua viliendelea.

b. Katika wiki ya mwisho ya mwezi Machi, vipindi vifupi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi ya Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Victoria.

c. Maeneo mengi ya nchi yanayopata mvua mara moja kwa mwaka yameendelea kupata mvua za '*Msimu*' kama ilivyotarajiwa, na mtawanyiko katika maeneo mengi umekuwa wa kuridhisha, isipokuwa katika maeneo machache ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) ambayo vipindi vya ukavu vilijitokeza husussan katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2019.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2019.

Mvua za Masika zimeendelea kunyesha vizuri katika wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2019 kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Victoria). Kutokea kwa kimbunga IDAI rasi ya Msumbiji (Magharibi mwa Madagascar) kumesababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kuwa hafifu na kupelekea upungufu mkubwa wa mvua katika maeneo mengi ya Nyanda za juu kaskazini mashariki na Pwani ya kaskazini katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2019. Aidha, mnamo wiki ya mwisho ya mwezi Machi, ongezeko la vipindi vya mvua lilijitokeza katika maeneo mengi ya

Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini na kanda ya ziwa Victoria.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2019

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa katika eneo la Kitropiki la Bahari ya Pasifiki, Mashariki mwa Bahari ya Hindi pamoja na maeneo ya kati Kusini mwa Bahari ya Hindi. Hali kadhalika, joto la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantic karibu na pwani ya Angola. Hali ya joto la juu kidogo ya wastani inalotarajiwa katika pwani ya Angola itapunguza msukumo wa unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2019

Ongezeko la vipindi vya mvua za Masika linatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi hususan wiki ya kwanza hadi ya tatu ya mwezi Aprili, 2019 ikifuatiwa na upungufu wa vipindi vya mvua katika wiki ya mwisho ya mwezi.

#### 2.2.1 Maeneo Yanayopata Misimu Miwili ya Mvua kwa Mwaka

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Ongezeko la vipindi vya mvua linatarajiwa katika maeneo mengi katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi Aprili, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika wiki ya tatu ya mwezi. Aidha vipindi vikavu kwa ujumla vinatarajiwa mnamo wiki ya mwisho ya mwezi hususan mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es salaam na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, ingawaje vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi Aprili, 2019, vikifuatiwa na ongezeko la vipindi vya mvua kwa maeneo mengi kati ya wiki ya pili na yatatu ya mwezi Aprili, na kufuatiwa na upungufu wa mvua katika wiki ya mwisho ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki tatu za mwanzo wa mwezi, vikifuatiwa na vipindi vichache vya mvua kwa maeneo machache katika wiki ya mwisho ya mwezi Aprili.

**2.2.2 Maeneo Yanayopata Msimu Mmoja wa Mvua kwa Mwaka**

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2019, ikifuatiwa na upungufu katika wiki zilizosalia.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Aprili, 2019. Aidha vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa katika wiki mbili za mwisho wa mwezi zilizosalia.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2019, ikifuatiwa na upungufu mkubwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo mengi katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi Aprili, 2019, ikifuatiwa na upungufu mkubwa katika wiki ya tatu na ya nne.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi Aprili, 2019, ikifuatiwa na upungufu mkubwa katika wiki ya tatu na ya nne.

**2.2 MATARAJIO KWA MWEZI MEI, 2019**

**Kwa ujumla kwa kipindi cha mwezi Mei, 2019 hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi nchini.**

Wataalam wakiwemo maafisa ugani katika sekta mbali mbali za uchumi ikiwemo kilimo wafuatilie na kupata taarifa za utabiri wa kila siku na siku kumi kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuwashauri wananchi ipasavyo ili kutumia vyema mvua zinazoendelea kunyesha katika mwezi huu wa Aprili.

Imetolewa na;
**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**